**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Shule ya Sekondari Mbugwe**
**S.L.P 266**
**BABATI,**

**Tarehe……………………**

**Mzazi/Mlezi wa …………. ..................**
**S.L.P ………**
**……………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MBUGWE HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MKOA WA MANYARA MWAKA……………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………. na atasoma tahasusi ya ……..……………………………………………………..…………………………………

Shule ya Sekondari Mbugwe ipo umbali wa Kilometa 40 Kaskazini mwa Mji wa Babati. Usafiri wa basi kutoka mjini Babati unapatikana katika kituo cha mabasi cha Babati mjini. Nauli ni Shilingi elfu mbili (2000).Muhula wa Masomo utaanza tarehe………….... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe………………...

**2.Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni sketi mbili za bluu nyeusi (dark blue) kwa Wasichana na suruali mbili za bluu nyeusi (dark blue) kwa Wavulana zenye marinda 2 kila upande na chini upana wa inchi 16.Sketi ziwe ndefu zinazogusa kifundo cha mguu na zenye marinda sita (6) kwa mpangilio wa 1 mbele,1 nyuma na 2 kulia na kushoto.(Rinda box).

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu kwa wavulana na wasichana.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kwa waislamu tu.Ifunike kifua cha mwanafunzi, pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni bukta moja na tisheti moja ya bluu isiyoashiria ushabiki wa timu yoyote na raba jozi moja kwa wasichana na kwa wavulana Bukta moja na T-shirt moja ya bluu isiyo na ushabiki wa timu yoyote (yaani isiyo na maandishi ) pamoja na Raba jozi moja .

v. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.Visiwe vya buti.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na soksi jozi mbili rangi nyeusi kwa wavulana.
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
viii. Sweta ya rangi ya bluu nyeusi (dark blue).
x. Nguo za kushindia ni suruali mbili za kijani kwa wavulana na sketi mbili za kijani kwa wasichana. Track suit jozi moja yenye rangi ya bluu nyeusi na mistari myeupe inayoshuka kutoka begani hadi chini kwa wavulana na wasichana.
xi. Tai ya bluu nyeusi (dark blue).
xii. Tisheti ya dark blue yenye nembo ya shule.Inapatikana shuleni kwa gharama ya mzazi.

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari makubwa (counter books quire four) yasiyopungua kumi na madaftari madogo ya msomi 10.
ii. **Rimu nne (A4)** kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi (combination) yako na viwe vya mtaala mpya.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology; (aje nayo au inapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 30,000/=)
v. Scientific Calculator (aje nayo au inapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 37000/=)
vi. Godoro size 2.5x3x6 (aje nalo au linapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 50,000/=)
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki kwa wasichana na bluu bahari kwa wavulana, na chandarua rangi ya bluu 1.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula vya bati (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2, moja ndogo (lita Kumi) na moja kubwa (lita 20) zenye mifuniko;
xi. Vifaa vya usafi:CBA na HGK: Alete panga lililonolewa, jembe lenye mpini, soft broom 1, squeezer 1 (mopper) pamoja na ufagio aina ya chelewa. PCB: Alete panga lililonolewa,jembe lenye mpini, hard broom 1, brash ngumu ya chooni pamoja na ufagio aina ya chelewa.
xii. Sabuni ya chooni lita tano (5) aina ya Dexi
xiii. Tochi kwa ajili ya mwanafunzi.
xiv. Faili (plastic file) moja kwa ajili ya kutunzia nyaraka za mwanafunzi.
xv. Alete nakala ya cheti cha kuzaliwa,form four results slip na leaving certificate.

**1.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha ya michango ya shule ilipwe kupitia akaunti **No.40701200073 NMB** Tawi la Babati. Jina la Akaunti ni **Mbugwe Shule ya Sekondari Reccurent.**

Unatakiwa kuleta Bank Pay in Slip (BPS) iliyoandikwa jina kamili la mwanafunzi na kidato chake. Siyo jina la mzazi wala mlezi.

**ANGALIZO;** Hatupokei fedha Taslimu. Fedha zikishawekwa katika akaunti ya shule hazirejeshwi.

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

i. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
ii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
iii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
iv. Kutunza mali za shule;
v. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
vi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwa sababu ya msiba au ugonjwa.
- Kila mwanafunzi aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu

**b. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na**:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
iii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
iv. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
v. Kufuga ndevu;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**c. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.Picha hizo zibandikwe kwenye jedwali hapo chini. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: ………………………………..**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………**

**NB:**

1. **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Mkuu wa shule 0783797453**
**Makamu Mkuu wa Shule 0764451570/0682024775**
**Mwandamizi Taaluma 0692731734/0763506838**
**Mwandamizi Nidhamu/Matron 0789566033, 0679892871**

2. **SIKU ZA WAZAZI/ WALEZI KUWATEMBELEA WANAFUNZI NI JUMAMOSI NA JUMAPILI ZA MWISHO WA MWEZI TU.**

**KIAMBATISHO B**

**OFISI WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI MBUGWE**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE MWAKA 2026/2027**

A. **MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Mbugwe. Pia nimesoma na kuelewa vyema sheria za shule. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu zifuatazo:- (Iwapo unakubali nafasi hii toa sababu vivyo hivyo kama unakataa nafasi toa sababu).

……………………………………………………………………………………

Tarehe ……………     saini ……………………………….

B. **MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………….mzazi/mlezi wa…………………………………

Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mbugwe, nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa. Aidha naahidi/siahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla. Kama unakataa eleza sababu:-

……………………………………………………………………………………

Ahsante

(i) Jina la mzazi/mlezi wa kiume ……………………………………………anwani……………….. Namba ya simu mkononi………………………………… tarehe……………….saini……………

(ii) Jina la mzazi/mlezi wa kike………………………………………… anwani …………………….. Namba ya simu ya mkononi…………………………tarehe…………………saini……………..

Ndugu/jamaa wanne (4) watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.

NB; **Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzii sipokuwa wazazi.**

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu/jamaa wa karibu ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo.

Jina la mzazi/mlezi……………………………………saini……………………..

| S/N | JINA (MAJINA MATATU) | PICHA (IBANDIKWE) | UHUSIANO WAKE NA MTOTO | ANWANI | SIMU YA MKONONI | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | |
| 2 | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | | | | | | |
| 4 | | | | | | |

*Kata isiyohusika*
**NB Sehemu “B” ijazwe na kusainiwa na mzazi/mlezi na si vinginevyo**

…………………
………………………
*MKUU WA SHULE*

**KIAMBATISHO. C**
**OFISI WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI MBUGWE**

**FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

**A. MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Mbugwe. Pia nimesoma na kuelewa vyema sheria za shule. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa nathibitisha/sithibitishi kutokushiriki migomo ya aina yoyote, fujo zozote na kosa lolote la jinai katika mazingira hii Mbugwe Sekondari (Iwapo unakataa mkataba huu toa sababu).

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Jina...................................................saini.................Tarehe............... ......

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi…………………….mzazi/mlezi wa……………………….…. Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mbugwe, nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Nimekubali na kumshauri mwanangu

kutoshiriki katika migomo ya aina yoyote, fujo zozote na jinai lolote awapo katika mazingira ya shule ya sekondari Mbugwe. Endapo atakiuka maelekezo haya, sheria za shule zichukue mkondo wake.

(Kama unakataa eleza sababu) …………………………………………………………
Mimi (Jina)……………………………… (mzazi/mlezi) wa ………………………………......
...(mwanafunzi) nathibitisha kauli hii.
Saini……………………………………. Tarehe……………………………………………...

**KIAMBATISHO. D**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MBUGWE SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Ref. No. MBG/ME/VOL. I…......
DATE…………………….
To the medical officer
……………………………….
……………………………….
GOVERNMENT HOSPITAL)
STUDENTS NAME……………………………….AGE……………..YEAR………………
Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for student if needed.

**………………………**
***JANETH G. KAAYA***
***THE HEADMISTRESS***

Medical certificate
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named student with regard to: -

**REMARKS**

1. SKIN.........................................................................................................................
2. EYES........................................................................................................................
3. TEETH……………………………………………………………………….....
4. B/S TEST (CH)...........................................................................................
5. PRESSURE……………………………………………………………….......
6. ABDOMEN………………………………………………………………
7. STOMACH………………………………………………………………
8. URINE……………………………………………………………………
9. HB. HAEMOGLOBIN……………………………………………………
10. TB TEST ………………………………………………………………
11. VDRI......................................................................................................................
12. HIVTEST………………………………………………………………
13. UPTTEST………………………………………………………………
14. STOOL…………………………………………………………………
15. ULCERS…………………………………………………………………
16. DIABETIC………………………………………………………………
17. ASTHMATIC……………………………………………………………
18. DISABILITIES (If Any) ..........................................................................................
19. ALLERGIES (If Any) ……………………………………………………….
20. ADDITIONAL INFORMATION (E.g. Any physical effects or impartment infections, chronic of family disease etc.) ……………………………………...

1. The student is in good health free from infection disease and is fit to proceed with studies……………………………………………………………………………………
2. The student will be attending treatment for …………………………………………

Signature …………………...........

Designation ………………………

Station…………………………….

**NOTE**: **MEDICAL OFFICER**

At the time of examination, please treat the individual for any ailment you note.

**RANGI NA MTINDO WA USHONAJI WA SARE YA SHULE NI KAMA INAVYOONEKANA KWENYE PICHA HAPA CHINI**

| | |
|---|---|
|  |  |
| **SARE ZA KUSHINDIA** | **SARE ZA DARASANI** |